بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

✦ ✦ ✦

# PONGWE ISLAMIC GIRLS SECONDARY SCHOOL

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

School Joining Instructions — 2027

## 1.0 UTANGULIZI

Shule ya Wasichana ya Kiislamu ya Pongwe ni shule ya bweni kwa wasichana pekee inayotoa elimu ya kuanzia Kidato cha I – IV. Shule ipo Tanga Mjini, umbali wa kilometa mbili (2) kutoka Pongwe karibu na Shule ya Msingi Maranzara. Usafiri wa pikipiki au bajaji unapatikana kutoka kituo cha basi Pongwe (Barabara ya Tanga–Segera) kwa gharama ya Tsh 2,000/=. au 3,000/=

### 1.1 Dhamira na Lengo la Shule

- Kuwawezesha mabinti wa Kiislamu kuitambua hadhi na majukumu yao katika jamii.
- Kuwaelimisha na kuwalea mabinti ili kupata viongozi bora wa baadae ngazi ya familia na taifa.
- Kujenga msingi imara wa wataalamu wa kike katika fani za sayansi ikiwemo utabibu.

### 1.2 Masomo Yanayofundishwa

Shule inafuata mtaala wa wizara ya elimu, sayansi na teknolojia - *mkondo wa jumla*. Masomo ni:

- Elimu ya Dini ya Kiislamu, Mathematics, English, Arabic, Physics, Chemistry, Biology, History, Geography, Kiswahili, Historia ya Tanzania na Maadili, Business Studies, Computer Science.

**⚠ Mfumo wa Kidijitali (TEHAMA)**

- Masomo 10 ya mtaala hufundishwa kwa njia ya mtandao kila mwanafunzi na kishikwambi.
- Kila mwanafunzi anapewa Kishikwambi kwa ushirikiano na Opportunity Education.

**⚠ Elimu ya Dini na Madrasa**

- *Qur’an (Hifdh na Tilawat), Hadith, Tawheed, Fiqh na Sirat* kwa lugha ya Kiarabu.
- Kila mwanafunzi LAZIMA asome Qur'an na EDK kwa miaka yote minne.

## 2.0 SARE ZA SHULE NA MAVAZI

Sare zote zinashonwa shuleni ili kuepusha mchanganyiko wa rangi na mitindo. Mwanafunzi haruhusiwi kushona sare nje ya shule.

| AINA YA SARE | VIPENGELE | RANGI / MAELEZO |
|---|---|---|
| Sare ya Darasani | Suruali 2 (Panjabi) Nusu Kanzu 2 (mikono mirefu) Ushungi mkubwa (chini ya goti) Baibui 1 | Darkish Blue, Nyeupe zinapatikana shuleni |
| Sare ya Nje (Shamba Dress) | Baibui refu, Ushungi mkubwa (chini ya goti), Suruali (Panjabi) na Sweta la kufuma kwa baridi. | Blue Masai. Sweta aje nalo Bluu (kufuma). |
| Viatu & Soksi | Viatu vya ngozi vyeusi (kamba) Soksi nyeupe (Jozi 2) Simple Raba za kushindia (Maruni) | Aje navyo |

Pia ni lazima kuja na: Baibui na shungi nyeusi za kuvaa kwa muda akisubiri sare zake zishonwe.

## 3.0 MAHITAJI YA BWENI, KITAALUMA NA USAFI

### 3.1 Vifaa Vinavyotolewa na Shule

(Gharama imo katika jedwali la Michango - Sehemu 5.2)

- Godoro futi 3/6 upana inch 4, Chandarua
- Shuka mbili (Blue Bahari na Pink)
- Sanduku la Chuma (Trunk)
- Daftari 15 (Quire 3 × 10, Quire 4 × 5), Rimu ya A4 na ya mistari, Graph paper 2
- Mkebe wa hesabu, Seti ya penseli za rangi na kalamu za wino.
- Vyombo: Ndoo, beseni, sahani, kikombe, kijiko, chupa ya chai, chupa ya maji ya kunywa.
- Jembe lenye mpini

### 3.2 Vifaa vya Binafsi (Kuja Navyo Siku ya Kuripoti)

- Taulo, malapa, mswaki, chupa ya maji ya moto
- Sabuni za kufulia, kuogea, mswaki na dawa ya meno.
- Mkoba wa madaftari (Begi Jeusi)
- Ufagio wa ndani (Soft broom) 1 na ufagio wa nje (Hard broom/Reki) 1
- Msahafu - chapa ya Saudi
- Daftari 6 za msomi kwa ajili ya masomo ya madrsa

> ⚠ **Tanbihi Muhimu**
> - *Mwanafunzi anapoacha au kuhama shule, ni lazima aondoke na vifaa vyake vyote binafsi ikiwemo godoro na sanduku.*

## 4.0 KANUNI NA SHERIA ZA SHULE

Shule imejengwa katika misingi ya uchamungu, nidhamu na uwajibikaji kwa mujibu wa maadili ya Kiislamu na sheria za nchi.

### 4.1 Maadili, Sare na Muonekano

- Mwanafunzi lazima ajisitiri na kuvaa sare rasmi ipasavyo wakati wote.
- Mapambo **HAYARUHUSIWI**: pete, bangili, hereni, rangi za kucha/hina/piko, nywele bandia.
- Lugha chafu, matusi, vurugu, dharau na nguo za kubana zimepigwa **MARUFUKU** kabisa.
- Usafi wa mwili, mavazi na mazingira ni wajibu wa kila mwanafunzi.

### 4.2 Mahudhurio, Masomo na Teknolojia

- Mahudhurio ya chini ya 81% yatapelekea kuzuiwa kufanya mtihani au kupanda darasa.
- Utoro wa siku 21 mfululizo ni sawa na kujiondoa shuleni.
- Vishikwambi vitatumika kwa masomo pekee - matumizi mabaya ya mitandao ni MARUFUKU.

> ⚠ **Kigezo cha Taaluma - Kupanda Darasa**
> - Wastani wa 55% unahitajika ili kupanda Kidato cha Pili na C - 7 kuingia Kidato cha Nne.
> - Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ufaulu unasisitizwa kiwango cha Daraja 'B' au zaidi.

### 4.3 Kanuni za Bweni na Ziara

- Kutoroka au kutoka nje ya shule bila kibali ni kosa kubwa.
- Kulala zaidi ya mtu mmoja kwenye kitanda kimoja ni MARUFUKU.
- Wazazi wanaruhusiwa kutembelea watoto Jumapili ya MWISHO WA MWEZI pekee.
- Ni marufuku kabisa kumletea mwanafunzi chakula cha aina yoyote.

### 4.4 Makosa Yanayopelekea Kufukuzwa Shule

- Matumizi ya pombe au dawa za kulevya
- Uzinzi au uasherati
- Wizi, udanganyifu, au kughushi
- Kutoroka au kuruka ukuta
- Vurugu au kupigana
- Kutishia usalama wa walimu au wanafunzi
- Kuharibu mali ya shule
- Kukataa ibada (kuacha swala)

> ⚠ **Tanbihi - Marejesho ya Fedha**
> - *Shule HAITARUDISHA fedha yoyote iwapo mwanafunzi atafukuzwa kwa utovu wa nidhamu.*

## 5.0 ADA, MICHANGO NA TARATIBU ZA BENKI

### 5.1 Ada ya Shule inalipwa kwa Awamu Tatu kulingana na Kidato husika.

| | | MGAWANYO WA MALIPO KWA DARASA (Tsh) | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| AWAMU | MWEZI WA KULIPA | KIDATO I | KIDATO II | KIDATO III | KIDATO IV |
| Awamu ya 1 | Januari | 800,000/= | 900,000/= | 850,000/= | 900,000/= |
| Awamu ya 2 | Aprili | 700,000/= | 800,000/= | 700,000/= | 800,000/= |
| Awamu ya 3 | Julai | 500,000/= | 450,000/= | 500,000/= | 450,000/= |
| JUMLA KUU | | 2,000,000/= | 2,150,000/= | 2,050,000/= | 2,150,000/= |

### 5.2 Gharama za Upimaji na Mitihani Kwa Watahiniwa Kidato II na IV.

| DARASA | AINA YA MITIHANI - 2027 | KIASI (Tsh) |
|---|---|---|
| Kidato II | Monthly Tests, Mock, Inter Islamic, Pre-FTNA na FTNA | 110,000/= |
| Kidato IV | Monthly Tests, Pre-MOCK, Mock, Inter Islamic, Pre-NECTA na CSEE | 165,000/= |

## 5.2 Michango Mingine ya Lazima

| AINA YA MCHANGO | KIASI (Tsh) |
|---|---|
| Vifaa vya Masomo na Bweni (Jedwali 3.1) Kwa anayetaka kulipia shuleni | **255,000/=** |
| Michango ya Shule (*Sare jozi 4, usajili, nembo, ID, ukaguzi, michezo, ukarabati n.k.*) | **320,000/=** |
| Bima ya Afya (NHIF) kwa ambao HAWANA ni LAZIMA | **55,000/=** |
| Mchango wa Kishikwambi ya mwanafunzi, Internet na Kompyuta | **300,000/=** |
| **JUMLA YA MICHANGO (Inalipwa Awamu ya kwanza anaporipoti)** | **930,000/=** |

## 5.3 Akaunti za Benki

| ✦ Jina la Akaunti: Pongwe Islamic Girls Secondary School ✦ | | |
|---|---|---|
| **BENKI** | **NAMBA YA AKAUNTI** | **MATUMIZI** |
| **CRDB Bank** | **0150705966600** | Ada ya Shule (Tuition) Pekee |
| **DTB Bank** | **0035678001** | Ada ya Shule (Tuition) Pekee |
| **Amana Bank** | **008121053180001** | Michango Yote (All Contributions) |

—— ❖ —— ✦ —— ❖ ——

# 6.0 UTARATIBU SIKU YA KURIPOTI

### TAREHE YA KURIPOTI KIDATO I

## Jumamosi, 02 Januari 2027

Saa 07:30 Mchana — 12:00 Jioni

—— ❖ —— ✦ —— ❖ ——

Mwanafunzi LAZIMA aje na Mzazi / Mlezi wake

## Nyaraka Zinazohitajika Siku ya Kuripoti

- Fomu ya utambulisho iliyojazwa (**Kiambatanisho A**)
- Fomu ya uchunguzi wa afya kutoka kwa daktari (**Kiambatanisho B**)
- Mkataba wa Mzazi Kukubali Kanuni na Taratibu za shule (**Kiambatanisho C**)
- Stakabadhi halisi za malipo ya **Benki (Pay-in Slips)** za ada na michango yote.
- **Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa** majina yafanane na majina yaliyosajiliwa katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi.

—— ❖ —— ✦ —— ❖ ——

**"Malezi Bora na Elimu Imara kwa Mustakabali wa Binti wa Kiislamu"**

—— ❖ —— اللَّهُمَّ آمِين —— ❖ ——